# Vunja UKIMYA Ondoa VIKWAZO!

## Unawezaje kufanya Elimu kuwa Salama kwa Wasichana?

**Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia**

**Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia 2016**

**Karatasi Kazi ya Kampeni**

GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum•Fostering Activism

### Utangulizi

*Vunja Ukimya, Ondoa Vikwazo! Unawezaje Kufanya Elimu Kuwa Salama Kwa Wasichana?* ni kauli mbiu ya siku 16 za kampeni ya uanaharakati. Kampeni ya kimataifa ya mwaka huu inayoadhimisha miaka 25 ya uwepo wake itaendelea kuonyesha uhusiano wake kati ya ukatili wa kijinsia na matumizi ya kijeshi, yanayoambatana na mfumo dume wenye ubaguzi na kujikita na uhusiano wake na matumizi ya mamlaka.

Kauli mbiu ya kampeni inalenga kufanya elimu kuwa salama kwa wote, hususani kwa wasichana na wanawake vijana, kwa kuainisha muundo wa kibaguzi kwa wanawake na wasichana katika mfumo wa elimu kuanzia majumbani, katika jamii, na mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na sera za serikali ambazo huathiri wasichana mashuleni. Kampeni itaanza tarehe 25 Novemba hadi tarehe 10 Desemba mwaka 2016.

Tunakuhimiza kutumia fursa hii Kuvunja Ukimya katika jamii yako. Wakati wa siku hizi 16 tutajenga uelewa miongoni mwa jamii, shule na sekta mbalimbali za serikali kuhusu vikwazo ambavyo vinazuia wanawake na wasichana kupata fursa ya elimu na kumaliza masomo yao.

Lengo na madhumuni ya karatasi kazi hii ni kupanga, kuiweka katika mazingira yanayotuzunguka na kufafanua madai yetu ya kimkakati kwa kutumia kampeni ya kikanda kuhusiana na masuala ya utetezi. Tafadhali kumbuka: kukamilisha karatasi kazi hii inapaswa iwe shughuli ya kwanza kabisa na ifanyike vizuri, kabla ya kuanza kampeni. Kama una matatizo katika matumizi ya karatasi kazi hii tafadhali wasiliana na **info@preventgbvfrica.org** kwa msaada zaidi.

### Jinsi ya Kutumia Karatasi Kazi Hii:

1. Soma nyaraka za mapitio ya kampeni na 'Karatasi kazi ya Kampeni' kwa makini
2. Kama mhusika mkuu unayeongoza siku 16 za kampeni kwenye shirika lako soma na kusanya taarifa ndani ya kifungu cha 'karatasi kazi' hakikisha unatafuta taarifa muhimu kutoka mashuleni, viongozi wa serikali na machapisho (unaweza kuwaomba wenzako wakusaidie kuandaa taarifa hii)
3. Andaa mkutano na wafanyakazi wenzako kwa ajili ya siku 16 za kampeni (ikiwezekana, ni vizuri iwe mapema kabla ya tarehe 25 Novemba ambapo kampeni inatarajiwa kuanza)
4. Kwenye mkutano utakaofanya na wenzako washirikishe taarifa ulizokusanya katika kipengele namba 2 hapo juu
5. Wagawe wafanyakazi katika makundi na fanya jaribio la kwanza la kujibu maswali katika jedwali hapo chini ya kifungu 'Karatasi kazi' (hakikisha unajibu 'Hatua Zinazohitajika' kwa kina, hii itasaidia kupanga mpango mahsusi wa kazi na wenye ufanisi)
6. Soma na jadili masuala ya utetezi ya kampeni kwa undani na chagua moja ambalo wewe (kama shirika) unaweza kuliwakilisha kwa ajili ya majadiliano zaidi katika jamii yako
7. Kubalianeni kuhusu malengo mnayotaka kutimiza katika kipindi cha kampeni na nini kitaashiria kuwa malengo mliyoyachagua yamefikiwa
8. Wote kwa pamoja na wenzake, tengenezeni mpango kazi wa kina wa kipindi cha kampeni. Hakikisha kwamba shughuli ulizopanga zinahusiana na malengo ambayo ungependa kuyatimiza. Tumia mwongozo wa shughuli za kampeni kwa ajili ya kupata mawazo zaidi
9. Sasa upo tayari kuanza kampeni yako, vunja ukimya kwa kubainisha vikwazo vya elimu kwa wasichana na shinikiza hatua zichukuliwe!

## Masuala ya Kampeni

Mwaka huu, kampeni ya Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia utalenga kuuliza maswali kwa jamii, wazazi, mashuleni na watunga sera ili kuwezesha upatikanaji wa elimu salama kwa wasichana na wanawake. Tutavunja ukimya kwa kuibua na kuweka wazi masuala ya majumbani mwetu, mashule na katika jamii ambayo yanasababisha vikwazo kwa wanawake na wasichana katika upatikanaji wa elimu na masuala ambayo yanafanya mazingira ya elimu kutokua salama.

Chagua kati ya masuala yaliyoainishwa mojawapo kati ya hayo au mchanganyiko wa masuala yafuatayo **(upatikanaji**, **usalama na masuala ya mifumo)** yanayosababisha vikwazo vya elimu kwa wasichana katika jamii yenu (elezea hapo chini). Panga kampeni yako kwa kuzingatia masuala uliyochagua ambayo unahitaji hatua zichukuliwe.

1. **Upatikanaji wa Elimu:** wasichana na wanawake vijana wanapaswa kupata elimu sawa na wavulana na wanaume vijana. Hii ni pamoja na familia kuwaandikisha wasichana shuleni na kuwasaidia kuzingatia masomo yao na kuhakikisha wasichana wanabaki mashuleni badala ya kuwaozesha

2. **Usalama Shuleni:** wasichana wana mahitaji maalum ambayo lazima yatatuliwe kwenye mazingira ya shule, kwa mfano, vifaa vya chooni, vifaa vya kujihifadhi wakati wa hedhi na awepo mfanyakazi mwenye jukumu la kushughulikia mahitaji haya. Halikadhalika kuondoa athari za kiusalama ambazo wasichana hukumbana nazo wakielekea shuleni

3. **Mfumo wa Elimu:** ndani ya mfumo wa elimu katika sera na utekelezaji kuna mifumo ambao inachangia kuwepo na ubaguzi hasi na kutokuwepo na usawa katika matumizi ya mamlaka kwa wasichana. Kuhakikisha mitaala na vitabu vya kiada vinahamasisha na kuzingatia usawa wa kijinsia.

## Karatasi Kazi:

Baada ya kuchagua suala ambalo ungependa kulionyesha wakati wa siku 16 za kampeni soma maswali hapo chini na tafuta taarifa muhimu ili uweze kukamilisha na kurekebisha kampeni yako kulingana na mahitaji muhimu zaidi katika jamii yako. Tumia majibu yako kukamilisha mpango kazi wa kipindi cha kampeni

| Masuala ya kampeni | Maswali ya karatasi kazi | Majibu (tafadhali kamilisha sehemu hii) | Hatua zinazohitajika kuchukuliwa na nani wa kuwasilisha suala hilo katika jamii yako (tafadhali kamilisha sehemu hii) |
|---|---|---|---|
| **Upatikanaji wa Elimu** | Je, wasichana na wanawake vijana wanapata fursa ya kwenda shule katika hali ya usawa katika jamii yako? | | |
| | Kuna idadi gani ya wanafunzi wa kike na wa kiume katika ngazi mbalimbali za elimu katika jamii yako? Je uwiano unabadilika katika ngazi ya elimu ya juu? Kwa nini? | | |
| | Je, kuna sera zozote ambazo ni za kibaguzi dhidi ya wasichana ( mfano. wasichana kufukuzwa wanapopata mimba, ukosefu wa faragha / usafi wa mazingira kwa wasichana, nk) | | |
| | Hata kama wasichana wanapata fursa ya elimu, je, wanaruhusiwa kumaliza shule? ni vikwazo gani vinavyowazuia wasichana kumaliza shule? | | |
| **Usalama Shuleni** | Je, ni vifaa gani vya shule vinavyopatikana (Ni kwa namna gani vinakidhi mahitaji maalum ya wasichana / wanawake vijana?) k.m ni utaratibu gani umewekwa kwa ajili ya kujihifadhi wakati wa hedhi? Kuna vyoo tofauti kwa wasichana na wavulana? | | |
| | Wasichana wanapokwenda shuleni ni athari zipi za kiusalama wanazokabiliana nazo katika jamii yako? kwa mfano. unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, utekaji nyara | | |

| Masuala ya kampeni | Maswali ya karatasi kazi | Majibu (tafadhali kamilisha sehemu hii) | Hatua zinazohitajika kuchukuliwa na nani wa kuwasilisha suala hilo katika jamii yako (tafadhali kamilisha sehemu hii) |
|---|---|---|---|
| **Mfumo wa Elimu** | Ni maudhui gani yanayofundishwa shuleni yanayochochea ubaguzi wa wasichana na wanawake vijana – na baadaye kuwanyima fursa ? (Je maudhui ya elimu yanapanda mbegu za kutokuwa na usawa wa mamlaka? Je inachochea fikra katika nchi ya kuwa wavulana wana thamani zaidi kuliko wasichana?) | | |
| | Je wasichana na wanawake vijana wanahamasishwa kushiriki kama vijana wenzao wa kiume? | | |
| | Je, wasichana na wanawake vijana wanafanyiwa unyanyasaji wa kijinsia / ukatili wa kingono kutoka kwa walimu na wanafunzi wengine? | | |